



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU  
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)



P.O Box 519,  
**DAR ES SALAAM.**  
Simu Na: +255- (0)22 -2760548/276055  
Nukushi Na: (022) 27605  
Barua pepe: [info@osha.go.tz](mailto:info@osha.go.tz)  
Simu Bila Malipo: 0800110091/0800110092

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUREJESHA MAFUNZO YA USALAMA NA AFYA KAZINI.**

**DAR ES SALAAM, Juni 05, 2020:**

Tunapenda kuwafahamisha wadau wetu wote na umma kwa ujumla kuwa tumerejesha huduma ya mafunzo ya Usalama na Afya mahali pa kazi ambayo hutolewa na OSHA baada ya kuyasitisha kwa muda kutokana zuio la mikusanyiko lililotolewa na serikali ili kudhibiti kusambaa kwa virusi vya Corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu (COVID-19).

Hivyo, kutokana na serikali kuruhusu shughuli za kielimu kuendelea baada ya kiwango cha maambukizi kupungua na wagonjwa wengi kupona, hali kadhalika OSHA tumerejesha huduma hii muhimu ambayo imekuwa ikisubiriwa na wadau wetu kwa kipindi chote tangu tulipoisitisha.

Mafunzo haya yataanza kutolewa rasmi kuanzia Juni 15, 2020 katika ofisi yetu ya Dar es Salaam pamoja na Kanda zetu zote kwa mujibu wa kalenda yetu ya mafunzo ya mwaka 2019/2020.

Aidha, OSHA inawakumbusha wadau wote watakaokuwa wanashiriki katika mafunzo yetu mbali mbali kuendelea kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na serikali katika kujikinga na virusi vya Corona ikiwemo kutoshikana mikono, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuvaa barakoa na kuepuka mikusanyiko mbali mbali.

Kwa upande wetu, tutahakikisha kwamba washiriki wa mafunzo wanakuwa salama kwa kuchukua tahadhari zote muhimu za kujikinga na virusi hivyo ikiwemo kuhakikisha kwamba kunakuwa na umbali unaokubalika (social distancing) baina ya washiriki katika vyumba vyetu vya mafunzo.

Tunawakaribisha sana kuwasilisha maombi na kushiriki katika kozi zetu mbali mbali.

*Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti yetu ([www.osha.go.tz](http://www.osha.go.tz)) na mitandao yetu ya kijamii.*

Paul L. Gyuna

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO**

OSHA  
OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH AUTHORITY